CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA

P.O.Box 1125, DODOMA. Tel: 026 – 2961101, Fax: 026 – 2961100,
E – Mail: info@lgti.ac.tz & Website: www.lgti.ac.tz

Tarehe: 27 Februari, 2019

Kwa mafundi wote walioshiriki katika mchakato wa Zabuni.

YAH: TAARIFA YA KUSUDIO LA KUTUNUKU ZABUNI.

Tafadhari rejea mada tajwa hapo juu.

Kufuatia Mwaliko wa Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/01; Kwa ajili ya kupata fundi sanifu wa kujenga darasa lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi mia (400) na Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/02; Kwa ajili ya kupata fundi sanifu wa kufunga na kuweka umeme katika Darasa lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi mia nne (400) zilizotangazwa tarehe 11 Februari, 2019 mpaka tarehe 18 Februari, 2019 katika mbao mbalimbali za matangazo na Tovuti ya Chuo Cha Serikali za Mitaa – Hombolo.

Chuo cha Serikali Za Mitaa kupitia maamuzi ya kikao cha Bodi ya Zabuni kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2019 inakusudia kutunuku Zabuni kama ifuatavyo;

i. Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/01 ametunukiwa **M/s Hassan R. Mvungi, S.L.P 1705, DODOMA** kwa gharama ya **Shilingi Milioni Thelathini Mia Nane Thelathini na Tisa Elfu tu** (Sh. **30,839,000.00**).
ii. Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/02 Mafundi sanifu wote waliowasilisha Zabuni zao hawakukidhi vigezo hivyo kukosa fundi sanifu katika kazi ya kufunga na kuweka umeme.

Scanned by CamScanner

Kwa mujibu wa kifungu 60(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 na kifungu 231(2) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma – Tangazo la Serikali Na. 446 la mwaka 2013 pamoja na marekebisho ya mwaka 2016, Chuo kinapenda kuwataarifu mafundi sanifu wote walioshiriki katika zoezi zima la mchakato wa Zabuni kwamba matokeo na maamuzi ya tunuku ya Zabuni ni kama yanavyoonekena hapo chini pia majina na sababu zilizosababisha kutokidhi vigezo kwa mafundi sanifu imeorodheshwa katika jedwali hapo chini. Hivyo, barua za tunuku kwa washindi zitatolewa baada ya siku saba toka tarehe ya tangazo hili.

Orodha ya Washiriki na sababu zilizopelekea kushindwa kukidhi vigezo vya Zabuni;

Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/01		
Na.	**Jina la Fundi**	**Sababu za kutokidhi vigezo**
01	M/s Francis Rwezaura.	Fomu ya bei haikujazwa kipengele A, D, E, F katika uk 7 na kipengele E katika uk 10 kinyume na maelekezo kwa wazabuni (Rejea kifungu Na.2.1) na hana uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali (Rejea kifungu Na. 2.2).
02	M/s Robert Makapi, S.L.P 1719, **DODOMA.**	Amekidhi vigezo vyote na kuwa mshindi wa Tatu (3) kwa mlinganisho wa gharama ya ujenzi.
03	M/s Joel Workshop Organisation.	Fomu ya kuwasilisha zabuni (Rejea kifungu Na. 5); Hajathibitisha uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali (Rejea kifungu Na. 2.2); Hajathibitisha elimu ya ufundi (Rejea kifungu Na. 2.3); Hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9) na Hajathibitisha udhamini katika zabuni (Rejea kifungu Na. 5)
04	M/s Dastan K. Ngemera, S.L.P 1023, **DODOMA**.	Fomu ya bei haikujazwa kipengele C, E, H,I katika uk 7 na kipengele B katika uk 8. (Rejea kifungu Na.2.1).
05	M/s Issa Mrutu.	Fomu ya bei haikujazwa kipengele E,G katika uk 8; C,A,B,C,D,E,F,G,H,I,J,K katika uk 9; E,D katika uk 10 na kipengele A,B,C,D,E katika uk 11 (Rejea kifungu Na.2.1); Hajathibitisha elimu ya ufundi (Rejea kifungu Na. 2.3) na pia Hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9).
06	M/s Said M. Ngwelo.	Fomu ya bei haikujazwa kipengele C, F, G, H, I, J katika uk 9 (Rejea kifungu Na.2.1) na pia hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za

Scanned by CamScanner

Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/01		
Na.	**Jina la Fundi**	**Sababu za kutokidhi vigezo**
		kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9).
07	M/s Ramadhan M. Feka.	Fomu ya kuwasilisha zabuni imefutwa bila kuwekwa saini (Rejea kifungu Na.2.1) na pia hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9).
08	M/s Malendi Entreprises, S.L.P 155, **DODOMA.**	Hajathibitisha uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali (Rejea kifungu Na. 2.2); hajathibitisha elimu ya ufundi (Rejea kifungu Na. 2.3); Hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9) na hajathibitisha udhamini katika zabuni (Rejea kifungu Na. 5)
09	M/s Bashiri J. Kiwenge, S.L.P 167, **DODOMA.**	Amekidhi vigezo vyote na kuwa mshindi wa pili (2) kwa mlinganisho wa gharama ya ujenzi.

Zabuni Na. PA/080/2018/2019/W/02		
Na.	**Jina la Fundi**	**Sababu za kutokidhi vigezo**
01	M/s Alex Mnyaonga.	Hajathibitisha uzoefu wa kufanya kazi yoyote ya umeme katika majengo ya Serikali (Rejea kifungu Na. 2.2); hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa za kibenki (Rejea kifungu Na. 2.9) na hajathibitisha udhamini katika zabuni (Rejea kifungu Na. 5).
02	M/s Jackson B. Lesiwa, S.L.P 5043, **DODOMA.**	Hajathibitisha uzoefu wa kufanya kazi yoyote ya umeme katika majengo ya Serikali badala yake ameonesha kazi za ujenzi tu (Rejea kifungu Na. 2.2); hajathibitisha uwepo wa akaunti au taarifa ya Benki (Rejea kifungu Na. 2.9) na hajathibitisha udhamini katika zabuni (Rejea kifungu Na. 5).

Uongozi wa Chuo unashukuru kwa ushirikiano mliouonesha katika kuitikia zabuni tajwa hapo juu, pia tunawakaribisha tena kushiriki katika fursa za zabuni mbalimbali pindi zitakazokuwa zimetangazwa na Chuo.

Dkt. Mpamila Madale

MKUU WA CHUO

Mkuu wa Chuo
Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo
S. L. P. 1125,
DODOMA

Scanned by CamScanner